YALIYOMO

A. UTANGULIZI 1

B. HALI YA UCHUMI NA MAENDELEO 5

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2015/16: 6

MAPITIO YA MAPATO, ... 6
MAPATO YA KODI 8
MAPATO YASIYO YA KODI 9
MIKOPO YA NDANI 9
MAPATO YA NJE 9
MAPITIO YA MATUMIZI 10

D. UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 12

ADA YA VIWANJA VYA NDEGE NA BANDARI (SHERIA YA ADA YA BANDARI NAMBA 2 YA MWAKA 1999) 13
KUFANYA MAPITIO YA VIWANGO VYA ADA NA TOZO MBALIMABLI ZINAZOTOZWA NA TAASISI ZA SERIKALI. 14
SHERIA YA BIASHARA (ADA YA UINGIZAJI WA MAGARI) 15

E. DENI LA TAIFA 15

F. MUSTAKABALI WA UCHUMI NA MAPATO 16

MWELEKEO WA UCHUMI 16
MUSTAKABALI WA MAPATO 17

G. MWELEKEO WA BAJETI, 2016/17 18

MWELEKEO WA MAPATO: 19
MAPATO YA NDANI 19
MAPATO YA NJE 19
MWELEKEO WA MATUMIZI 21

H. HATUA ZA KUBANA MATUMIZI 26
MATUMIZI YA KAWAIDA 26
KUTEKELEZA MIRADI YA MAENDELEO YENYE TIJA ZAIDI 27
KUDHIBITI GHARAMA KUTOKANA NA KUANZISHWA TAASISI MPYA 28
MATUMIZI YA KODI YA MIUNDOMBINU (INFRASTRUCTURE TAX) 28
I. HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO 30
UANZISHAJI NA USIMAMIZI WA MAENEO MAALUM YA KIKODI (BLOCK MANAGEMENT SYSTEM): 31
KUHAKIKISHA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA KODI YA ARDHI NA MAJENGO (PROPERTY TAX): 32
KUYAFANYIA KAZI MAPENDEKEZO YA KUONGEZA MAPATO YALIYOIBULIWA KATIKA MAABARA YA MAPATO: 32
KUONGEZA UDHIBITI WA MISAMAHA YA KODI: 33
KUPAMBANA NA MAGENDO YA MAFUTA: 33
HATUA ZA KIUTAWALA 33
VIBALI VYA KODI KWA WAZABUNI (INCOME TAX CLEARANCE CERTIFICATE) 34
USAJILI WA JINA LA BIASHARA (BUSINESS REGISTRATION NAME) 35
USIMAMIZI WA MAPATO KUTOKANA NA ARDHI: 35
UHAULISHAJI MAGARI KUTOKA ZANZIBAR KWENDA TANZANIA BARA 36
USAJILI WA VYOMBO VYA MOTO 36
SURA YA BAJETI 37
J. SHUKRANI 38
K. HITIMISHO: 41

HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO MHESHIMIWA DKT. KHALID SALUM MOHAMED

KUHUSU MWELEKEO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI, MEI 18, 2016.

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati Maalum ya kujadili mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

2. **Mheshimiwa Spika,** Niruhusu nianze, kama ilivyo ada yetu waumini, kwa kumshukuru na kumdhukuru Mola wetu muumba kwa neema zake zote anazoendelea kuturuzuku, ikiwemo ya uhai, afya njema, amani na utulivu. Ni kwa neema hizi ambazo nyingi hatuna uwezo nazo, ndio leo hii tumeweza kukutana hapa. Kukutana huku kutatuwezesha kutimiza matakwa ya Katiba yetu inayotutaka kujadili mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka unaofuata wa fedha, yakiwasilishwa na Waziri mwenye dhamana ya Fedha.

3. **Mheshimiwa Spika**, Naomba nichukue fursa hii kwa kuanza kutoa pongezi na shukrani. Kwanza, nianzie kwa kumpongeza sana Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais

wetu wa Zanzibar ambae pia ndie Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nampongeza Dkt. Shein kwa kuchaguliwa tena na Wananchi walio wengi kuiongoza tena nchi yetu kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Wote tunafahamu kuwa kuchaguliwa huku kunatokana na imani kubwa waliyonayo wananchi kwake, kutokana na kazi kubwa aliyoifanya katika awamu ya kwanza ya uongozi wake. Namuombea kipindi kingine cha utendaji uliotukuka, wenye uadilifu, hekima na mafanikio makubwa zaidi. Mwenyezi Mungu amuongoze kututumikia vyema wananchi sote, AMIN.

4. **Mheshimiwa Spika**, Niruhusu pia nimpongeze sana Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais, mosi, kwa kuendelea kuaminiwa mara hii na Wananchi wa Jimbo jipya la Mahonda. Kwa kumuamini na kumkubali kwao wamemchagua kuwa Muwakilishi wao katika chombo hiki muhimu kwa nchi yetu. Pili, nampongeza kwa kuendelea kupata imani ya Mheshimiwa Rais ambae amemteua tena kuwa Makamu wake wa Pili wa Rais. Namtakia utendaji thabiti, wa mafanikio na mfano kwetu sote.

5. **Mheshimiwa Spika**, Naomba pia nitumie fursa hii kukupongeza sana wewe binafsi kwa kuchaguliwa kushika nafasi hiyo ya kuliongoza Baraza letu hili la tisa. Nawe pia umepata imani ya Wajumbe wa Baraza hili na ni imani yangu kuwa katika kipindi chako tutashuhudia utendaji wa hali ya juu wa Baraza hili na kuimarika zaidi mahusiano yake na Mihimili mingine

ya dola; Mhimili wa Utendaji na Mahakama. Nakutakia kila la kheri.

6. **Mheshimiwa Spika**, Pongezi zangu za dhati zinakwenda pia kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili, waliochaguliwa na Wananchi, walioteuliwa kupitia viti maalum na walioteuliwa na Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa matakwa ya Katiba yetu. Nawapongeza pia Waheshimiwa wote waliopata fursa ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuziongoza Wizara mbalimbali. Nao wote nawatakia utendaji bora zaidi katika kuwahudumia Wananchi wote.

7. **Mheshimiwa Spika**, Pongezi zote hizi zinafuatia kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa marudio wa Machi 20 mwaka huu 2016, kutokana na matatizo yaliyojitokeza na kufutwa uchaguzi wa awali na Tume ya Uchaguzi. Uchaguzi Mkuu ulifanyika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Naomba pia nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuiongoza Jahmuri yetu ya Muungano kama Rais wake wa Tano tokea kuasisiwa kwa Muungano huo.

8. **Mheshimiwa Spika**, Tayari Mheshimiwa Magufuli amejipambanua kwa uchapaji kazi wake na kutovumilia uzembe, ubadhirifu na wizi wa mali za umma. Kwa hakika kaulimbiu yake ya “Hapa Kazi Tu” tayari imedhihirika katika vitendo vyake kwa kipindi kifupi cha uongozi wa nchi yetu.

Tunamuombea uongozi mwema na wa mafanikio, yeye na wasaidizi wake wakuu.

9. **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa shukrani, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimwia Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuniamini na kuniteua kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango, ambayo ndio roho na moyo wa maendeleo yetu. Shukrani pia ziende kwa Wananchi wote wa Zanzibar kwa utulivu wao mkubwa unaoonesha ukomavu wao kwa nyakati zote, hata pale penye majaribu ya kijamii na kisiasa kama ilivyojitokeza mara hii katika Uchaguzi wetu Mkuu. Bila ya shaka yoyote, napenda kuvishukuru vyama vyote vya siasa na viongozi wake, hususan Chama Cha Mapinduzi, kwa ustahamilivu mkubwa wa kisiasa na kuivusha salama Zanzibar katika kipindi hicho.

10. **Mheshimiwa Spika**, Zanzibar imeandika historia mpya ya siasa, Zanzibar imeandika zama mpya za utulivu, Zanzibar imeandika ukurasa mpya wa demokrasia, Naamini kuwa, kwa yeyote mwenye kutafakari kwa makini na bila ya kuegemea upande wowote, atabaini mafunzo mengi ya kisiasa, kidemokrasia na kijamii katika mambo ambayo tumepitia katika kipindi hicho mpaka kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa Marudio wa tarehe 20 Machi 2016 na hata baada ya hapo.

11. **Mheshimiwa Spika**, Niruhusu pia nitoe shukran za aina ya pekee kwa Wananchi wote wa Jimbo la Donge,

kwa kunichagua kwa kauli moja kuwawakilisha katika Baraza lako hili tukufu la kutunga Sheria. Nimepokea kwa unyenyekevu mkubwa uteuzi wa Mheshimiwa Rais na wa Wananchi wa Donge. Najua dhima niliyonayo na ninamuomba Allah kuniwezesha kwa kila hali kuwatumikia vyema wananchi wote wa Zanzibar kwa dhamana niliyopewa ya uwaziri wa Fedha na Mipango na ule wa Jimbo langu la Donge kwa dhamana ya kuwawakilisha katika Baraza hili.

12. **Mheshimiwa Spika**, Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nianze kwa kuwasilisha mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/16.

B. HALI YA UCHUMI NA MAENDELEO

13. **Mheshimiwa Spika**, asubuhi ya leo nilieleza mwenendo wa uchumi wetu kwa mwaka uliopita wakati nikiwasilisha Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2015. Sikusudii kurejea maelezo niliyoyatoa awali. Naomba tu niseme kuwa kwa mwaka 2015, pato letu la nchi limefikia TZS 2,308.0 bilioni kwa bei za mwaka huo sawa na TZS 1,169.0 bilioni kwa bei za kudumu za mwaka 2007. Kwa miaka mitano iliyopita, uchumi wetu umekuwa kwa wastani wa asilimia 7.0. Kwa bei za kudumu za mwaka 2007, wastani wa pato la mtu binafsi nao umefikia Dola 674 za Marekani, sawa na Dola 817 kwa bei za mwaka 2015. Wakati tukijipanga kuendeleza mageuzi ya kiuchumi,

tunapaswa kujua kuwa tunaanzia na kiwango hicho cha uchumi wetu.

14. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Ofisi yake ya Mtakwimu Mkuu imekamilisha Utafiti wa Kipato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2015. Kazi hii imehusisha pia wataalamu kutoka nje na ilianza na mapitio ya njia inayotumika kupima umaskini kwa kuzingatia hali halisi ya maisha ya Zanzibar. Matokeo ya awali yanaonesha mafanikio katika jitihada zetu za kupunguza umaskini, zikionesha kuwa wananchi wanaoishi chini ya kiwango cha mahitaji wamepungua kutoka asilimia 34.9 mwaka 2010 hadi asilimia 30.4 mwaka 2015. Aidha, watu wanaoishi kwa umaskini wa chakula wamepungua kutoka asilimia 11.7 hadi asilimia 10.8. Kiwilaya, bado jitihada zinahitajika zaidi kwa Wilaya ya Micheweni Pemba kwani imeendelea kuongoza ikifuatiwa na Wilaya nyengine za Pemba. Kiwango cha chini zaidi cha umaskini kwa sasa kimejitokeza katika Wilaya za Magharibi. Matokeo haya ya utafiti yanahitaji juhudi maalum katika miaka mitano ijayo.

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2015/16:

Mapitio Ya Mapato,

15. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2015/16, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya TZS 830.4 bilioni. Kati ya fedha hizo, TZS 450.5 bilioni ni mapato ya ndani na

TZS 349.9 bilioni kutokana na ruzuku na mikopo kutoka nje. Ili kuziba nakisi ya Bajeti, Serikali iliidhinisha kukopa ndani TZS 30.0 bilioni.

16. **Mheshimiwa Spika**, makusanyo halisi kwa kipindi cha miezi tisa hadi Machi 2016, yamefikia TZS 399.0 bilioni sawa na asilimia 48 ya makadirio ya mwaka.

17. **Mheshimiwa Spika**, Kati ya mapato hayo, jumla ya TZS 306.1 bilioni zimekusanywa kutokana na vyanzo vya ndani sawa na asilimia 68 ya lengo la miezi tisa. Ukusanyaji huu unamaanisha ongezeko la mapato ya ndani kwa TZS 31.1 bilioni ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 275.0 bilioni yaliyopatikana katika kipindi kama hicho hadi Machi 2015, sawa na ukuaji wa asilimia 11.3.

18. **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na ongezeko hilo la mapato, lengo la ukusanyaji kwa kipindi hicho halikufikiwa. Sababu kuu za kutofikia lengo la ukusanyaji ni pamoja na hizi zifuatazo:
    i. Kuchelewa kwa marejesho ya Kodi ya VAT kutoka SMT kwa sababu ya Sheria mpya ya VAT ya Tanzania Bara iliyofuta kipengele cha marejesho hayo;

    ii. Kupungua kwa uingizaji wa bidhaa nchini, hususan magari; na

    iii. Kupungua kwa idadi ya watalii waliotembelea Zanzibar kwa asilimia 5.7.

Mapato ya Kodi

19. **Mheshimiwa Spika**, Kati ya mapato ya ndani, mapato kutokana na kodi yamefikia TZS 288.5 bilioni, sawa na asilimia 88.8 ya lengo la TZS 324.9 bilioni. Ukusanyaji huo pia unaashiria ukuaji wa mapato kwa asilimia 19 sawa na TZS 46.0 bilioni kutoka TZS 242.5 bilioni zilizokusanywa hadi Machi mwaka 2015. Utendaji wa ZRB umefikia asilimia 85.4 ya lengo baada ya kukusanya TZS 141.3 bilioni wakati lengo lilikuwa ni TZS 165.4 bilioni. Athari niliyoeleza awali ya kutorejeshwa fedha za VAT kwa bidhaa zitokazo Tanzania Bara imejitokeza katika kiwango cha utendaji wa ZRB. Hali hii pia imepelekea ukuaji mdogo wa mapato wa asilimia 4.1 kutoka TZS 135.7 bilioni za mwaka jana.

20. **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa TRA, makusanyo halisi ya kodi kwa miezi tisa hadi Machi 2016 yamefikia TZS 121.0 bilioni, sawa na asilimia 91.4 ya lengo la kukusanya TZS 132.4 bilioni. Hata hivyo, ikilinganishwa na utendaji wa kipindi kama hicho kwa mwaka 2014/15, kunajitokeza ongezeko la asilimia 13.3 sawa na TZS 14.2 bilioni kutoka TZS 106.8 bilioni za mwaka jana. Kati ya makusanyo hayo, Idara ya Forodha imemudu kukusanya TZS 72.4 bilioni kati ya lengo la TZS 85.1 bilioni kwa kipindi hicho, sawa na utendaji wa asilimia 85.1. Idara ya Kodi za Ndani imeweza kuvuka lengo kwa kukusanya TZS 48.6 bilioni wakati lengo ni TZS 47. 3 bilioni.

Mapato yasiyo ya Kodi

21. **Mheshimiwa Spika**, Kati ya mapato ya ndani, Serikali ilitarajia kukusanya TZS 25.0 bilioni kutokana na mapato yasiyo ya kodi. Makusanyo halisi kutokana na Wizara mbalimbali za Serikali kwa kipindi cha miezi tisa yamefikia TZS 17.6 bilioni, sawa na asilimia 103 ya lengo la kukusanya kipindi hicho la TZS 17.0 bilioni. Ukusanyaji huo unamaanisha ukuaji wa mapato kutoka chanzo hicho kwa asilimia 5.4 ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa mwaka jana kipindi kama hicho ya TZS 16.7 bilioni.

Mikopo ya Ndani

22. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha miezi tisa, Julai hadi Machi 31 mwaka huu, Serikali imekopa ndani jumla ya TZS 10.0 bilioni, ikiwa ni asilimia 33 ya fursa ya kukopa TZS 30 bilioni iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kinashabihiana na mikopo ya kipindi kama hicho kwa mwaka wa 2014/15.

Mapato ya Nje

23. **Mheshimiwa Spika**, Mapato kutoka nje yalifikia TZS 82.8 bilioni. Jumla ya TZS 75.1 bilioni ni ruzuku na mikopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 22 tu ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo,

Ruzuku ni TZS 37.9 bilioni na Mikopo ni TZS 37.2 bilioni. Kiasi kilichobakia cha TZS 7.7 bilioni ni Misaada ya Kibajeti (GBS).

24. **Mheshimiwa Spika**, Kama inavyojitokeza, kwa ujumla, ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha mapitio umeathiriwa zaidi na mwenendo usioridhisha wa mapato ya nje uliosababishwa zaidi na kuendelea kusuasua kwa utekelezaji wa miradi mikubwa kama vile ujenzi wa jengo jipya la abiria la uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume Zanzibar, ujenzi wa barabara za Kati Unguja, na mradi wa kuimarisha usalama ikiwemo uwekaji wa Kamera za CCTV.

Mapitio ya Matumizi

25. **Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa mapato umeathiri utekelezaji wa Bajeti kimatumizi. Hadi Machi 31 mwaka 2016, matumizi halisi yalifikia TZS 352.9 bilioni, yakijumuisha TZS 298.4 bilioni za matumizi yatokanayo na mapato ya ndani na TZS 54.5 bilioni matumizi yatokanayo na mapato ya nje. Matumizi kwa ajili ya kazi za kawaida yalifikia TZS 283.8 bilioni, sawa na asilimia 66 ya lengo la mwaka kama ifuatavyo:

    i. Mishahara TZS 145.6 bilioni sawa na asilimia 71 ya makadirio ya mwaka;

    ii. Mfuko Mkuu wa Serikali TZS 66.5 bilioni sawa na asilimia 79 ya makadirio ya mwaka;

iii. Ruzuku kwa Taasisi mbalimbali TZS 36.0 bilioni sawa na asilimia 63; na

iv. Matumizi mengineyo TZS 35.6 bilioni sawa na asilimia 42 ya makisio ya mwaka.

26. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi hicho cha mapitio, matumizi ya kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo yamefikia jumla ya TZS 69.1 bilioni, sawa na asilimia 17 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, fedha kutokana na Washirika wa Maendeleo ni TZS 54.5 bilioni, sawa na asilimia 16 ya makadirio ya mwaka wakati mchango wa Serikali umefikia TZS 14.60 bilioni sawa na asilimia 28 ya makadirio.

Matarajio ya Mapato Julai – Juni 2015/2016.

27. **Mheshimiwa Spika**, Haitarajiwi kuwa Miradi mikubwa iliyopata changamoto wakati wa utekelezaji itapata ufumbuzi katika kipindi kilichobakia cha Bajeti. Kwa sababu hiyo, na kwa kuzingatia mwenendo wa mapato ya ndani, matarajio ya makusanyo ya mapato hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Juni 2016 ni kukusanya TZS 516.0 bilioni, sawa na asilimia 62 ya Bajeti ya mwaka ya TZS 830.4 bilioni.

28. **Mheshimiwa Spika**, Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia TZS 412.5 bilioni, sawa na asilimia 91.6 ya makisio ya TZS 450.5 bilioni. Kati ya kiasi hicho, TRA inatarajiwa kukusanya TZS 163.7 bilioni, sawa na asilimia 91.7 ya makadirio ya mwaka. Mapato

kutoka ZRB yanatarajiwa kufikia TZS 204.3 bilioni sawa na asilimia 90.4 na makusanyo ya Mawizara ni TZS 23.4 bilioni, sawa na asilimia 119.5. Kodi ya Mapato (PAYE) kutoka SMT inatarajiwa kufikia TZS 21.0 bilioni sawa na lengo.

29. **Mheshimiwa Spika**, Kutokana na sababu zilizoelezwa awali, mikopo na ruzuku kutoka nje inatarajiwa kufikia jumla ya TZS 84.3 bilioni sawa na asilimia 24 tu ya makadirio ya mwaka.

D. UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

30. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2015/16, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kuimarisha mapato ya ndani. Utekelezaji wa hatua hizo ni kama ifuatavyo:

Kodi ya Miundombinu (Infrastructure Tax)

31. **Mheshimiwa Spika**, Baraza la Wawakilishi liliidhinisha uanzishwaji wa kodi ya Miundombinu (Infrastructure Tax) kwa lengo la kuimarisha miundombinu nchini. Ada zifuatazo zimetekelezwa kama zilivyoidhinishwa:

i. Dola moja ya Kimarekani kwa siku kwa kila mgeni atakaelala katika hoteli za Zanzibar.

ii. TZS 2,000 kwa kila abiria anaeondoka katika Bandari za Zanzibar kwenda Katika Bandari nyengine za Tanzania nje ya Zanzibar, na TZS

1,000 kwa kila abiria anaeondoka katika Bandari za Zanzibar kwenda katika Bandari nyengine za Zanzibar.

iii. TZS 2,000 kwa kila abiria anaeondoka katika kiwanja cha ndege kilichopo Zanzibar na kwenda kiwanja chengine ndani ya Tanzania.

iv. Asilimia 3 ya thamani za bidhaa zinazoingizwa nchini.

v. Asilimia 2 katika mauzo ya umeme.

vi. TZS 100/= ya ziada kwa lita ya Petroli au Dizeli inayoingizwa nchini.

32. **Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, Bodi ya Mapato Zanzibar imefanikiwa kukusanya TZS10.5 bilioni sawa na asilimia 92 ya makadirio ya miezi tisa ya lengo la TZS 11.4 bilioni hadi kufikia Machi 2016. TRA kwa upande wake imekusanya jumla ya TZS 5.96 bilioni sawa na asilimia 79.5 ya lengo la TZS 7.5 bilioni kwa kipindi cha miezi tisa.

Ada ya viwanja vya ndege na Bandari (Sheria ya Ada ya Bandari Namba 2 ya Mwaka 1999)

33. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ili kuongeza rasmi ada hiyo kutoka Dola 8 za Kimarekani hadi kufikia Dola 9 za Kimarekani, ambayo tayari ilikuwa inatozwa na Kampuni za Ndege kwa kutumia Sheria ya Tanzania Bara. Hadi kufikia

Machi 2016, jumla ya TZS 4.47 bilioni zimekusanywa katika kianzio hicho ambacho ni sawa na ukuaji wa asilimia 45.6 ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 3.1 bilioni kwa mwaka uliopita katika kipindi kama hicho.

34. **Mheshimiwa Spika**, Aidha, Serikali imeongeza tozo la mauzo ya tiketi na usafirishaji wa mizigo baharini kutoka asilimia 5 ya kabla hadi asilimia 8 kama ilivyoidhinishwa. Hadi kufikia Machi 2016, jumla ya TZS 1.84 bilioni zimekusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 94.4 ya lengo la mwaka la TZS 1.95 bilioni.

Kufanya Mapitio ya Viwango vya Ada na Tozo mbalimabli zinazotozwa na Taasisi za Serikali.

35. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ilifanya mabadiliko ya viwango vya Ada na Tozo mbalimbali katika Taasisi zake, kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyokuwa ya kodi na kuvifanya viwango hivyo viendane na wakati. Hadi kufikia Machi 2016 jumla ya TZS 900 milioni zimekusanywa kutokana na mabadiliko ya viwango hivyo ikilinganishwa na lengo la TZS 600 milioni kwa miezi 9, sawa na asilimia 150 ya lengo.

36. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubali kuweka kiwango mbadala cha ama TZS 100,000 kwa gari au asilimia 3 ya thamani ya gari inayoingizwa kwa kufuata kiwango kinachotoa mapato zaidi. Jumla ya TZS 710 milioni zimekusanywa katika kipindi cha mapitio, sawa na asilimia 60.6 ya makadirio ya mwaka.

E. DENI LA TAIFA

37. **Mheshimiwa Spika**, Kutokana na mikopo mipya, malimbikizo ya deni la kiinua mgongo, wazabuni na kudhoofika kwa Shilingi ya Tanzania kwa kulinganisha na Dola ya Kimarekani, Deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 25.7 hadi TZS 398.6 bilioni mwisho wa mwezi wa Machi 2016 kutoka TZS 317.2 bilioni za Machi 2015. Deni la nje limekuwa kwa asilimia 26 kutoka TZS 211.8 bilioni hadi TZS 266.8 bilioni katika kipindi hicho. Aidha, deni la ndani nalo limekuwa kwa asilimia 31.1 kutoka TZS 99.3 bilioni hadi TZS 130.2 bilioni, likiathiriwa zaidi na malimbikizo ya deni la Kiinua mgongo na lile la Hati Fungani.

38. **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuongezeka huko kwa deni letu, bado kiwango hicho ni endelevu na kinachoashiria kuwa Serikali ina uwezo wa kulilipa. Kwa kulinganisha na Pato la Taifa, deni hilo ghafi ni

uwiano wa asilimia 17.3 tu ya Pato la Taifa la mwaka 2015.

F. MUSTAKABALI WA UCHUMI NA MAPATO
Mwelekeo wa Uchumi

39. **Mheshimiwa Spika**, Dira ya maendeleo ya kiuchumi imeelezwa vyema katika hotuba ya uzinduzi wa Baraza hili la tisa iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kimsingi, bado dira yetu ni kufikia uchumi wa kipato cha kati. Mheshimiwa Rais pia ameeleza haja ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi ili isipungue asilimia 8 kwa mwaka. Jitihada zetu zitaelekezwa katika kushajiisha uwekezaji, uimarishaji wa sekta za uchumi kama vile huduma, hususan utalii, mageuzi ya viwanda na kilimo, ikiwemo cha mazao, ufugaji na uvuvi.

40. **Mheshimiwa Spika**, Mageuzi haya ya kiuchumi yataletwa kupitia utekelezaji wa Mkakati mpya wa maendeleo uliochukua nafasi ya MKUZA II. Kama nilivyoeleza wakati wa kuwasilisha Mpango wa Maendeleo, moja ya eneo muhimu la matokeo katika Mkakati huo mpya ni la mageuzi ya kiuchumi. Mageuzi haya yanakusudia kuimarisha sekta zote hizo nilizozitaja kwa kuzingatia uhusiano wa sekta hizo katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi.

Mustakabali wa Mapato

41. **Mheshimiwa Spika**, Mustakabali wa mapato ya Serikali kwa miaka mitano ijayo umejikita zaidi katika kuimarisha uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani. Mwelekeo huu unaendana na dhamira ya Serikali ya kuongeza kujitegemea na kupunguza kadiri iwezekanavyo utegemezi wa Washirika wa Maendeleo katika kuhudumia Bajeti ya Serikali. Ni muhimu kuelewa kuwa hatufungi milango ya mashirikiano na Washirika wa Maendeleo. Mashirikiano na wao hayatasitishwa, na pale watakapotusaidia tutaendelea kupokea misaada. Hata hivyo, lengo kuu ni kujitegemea wenyewe. Katika Hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza hili, Mheshimiwa Rais alieleza kuwa lengo la Serikali ni kukusanya TZS 800 bilioni ifikapo mwaka 2020/21 kutokana na mapato ya ndani kutoka TZS 362.8 bilioni zilizokusanywa mwaka 2014/15.

42. **Mheshimiwa Spika**, Jitihada zinazochukuliwa kwa sasa ni kuhakikisha kuwa lengo hilo lililotamkwa na Mheshimiwa Rais sio tu kuwa linafikiwa bali linafikiwa mapema zaidi katika kipindi hicho, kabla ya mwaka 2020/21. Sisi tunaamini kuwa hili linawezekana. Wenye dhamana ya kulisimamia hili tunaahidi kutimiza wajibu wetu ili liwezekane.

G. MWELEKEO WA BAJETI, 2016/17

43. **Mheshimiwa Spika**, Bado nchi yetu ni maskini na wananchi wanaitegemea Serikali yao kuwaletea maendeleo na kuwatoa katika umaskini. Hali hii inahitaji kuendelea kuwekeza katika huduma muhimu za jamii na mageuzi ya kiuchumi. Ili kukidhi mahitaji haya ya jamii, lengo Kuu la Bajeti ya Serikali litaendelea kuwa ni kujenga jamii iliyoelimika, yenye siha na yenye uhakika wa chakula, uwezo wa kiuchumi na inayothamini na kufuata misingi ya utawala bora.

44. **Mheshimiwa Spika**, Matumizi ya Serikali yataendelea kuelekezwa katika kuimarisha na kuendeleza maeneo yaliyozingatiwa katika Bajeti iliyopita yakiwemo (i) huduma za Elimu (ii) Huduma za Afya na ustawi wa jamii (iii) Miundombinu ya msingi; na (iv) Utawala bora.

45. **Mheshimiwa Spika**, Mustakabali huo wa Bajeti umejiegemeza katika utekelezaji wa mambo yafuatayo:

    i. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015;

    ii. Mkakati mpya wa Maendeleo unaochukua nafasi ya MKUZA II unaozingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals – SDGs) na Mpango wa Mageuzi ya Kiuchumi;

iii. Dira na uono wa Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kama ilivyoelezwa katika Hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza hili la tisa la Wawakilishi tarehe 5 April 2016;

Mwelekeo wa Mapato:

Mapato ya Ndani

46. **Mheshimiwa Spika**, Jumla ya TZS 482.4 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kwa mwaka 2016/17 kutoka katika vianzio vya ndani kwa mchanganuo ufuatao:
    i. ZRB: inatarajiwa kukusanya TZS 237.4 bilioni
    ii. TRA: inatarajiwa kukusanya TZS 188.8 bilioni
    iii. Mapato ya mawizara: TZS 26.4 bilioni
    iv. Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT: TZS 21.0 bilioni
    v. Gawio la faida kutoka BOT: TZS 4.0 bilioni
    vi. Mgao wa faida kutoka kwenye Mashirika ya Serikali: TZS 4.8 bilioni.

Mapato ya Nje

47. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2016/17, Serikali inatarajia kupokea ruzuku ya TZS 93.3 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kukopa nje jumla ya TZS 231.5 bilioni na hivyo kufanya mapato kutoka nje kufikia TZS 324.8 bilioni. Aidha Serikali

inatarajia kupokea TZS 1.3 bilioni zikiwa ni fedha kutokana na misamaha ya madeni (MDRI).

48. **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na fedha hizo zinazotarajiwa kupatikana kwa ajili ya kutekeleza Programu na Miradi ya Maendeleo, miradi ifuatayo imefikia hatua za mwisho za maandalizi na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwaka ujao wa fedha baada ya kuidhinishwa rasmi. Kwa sasa Miradi hiyo inaoneshwa katika Bajeti kwa utaratibu wa 100T ili kuepusha haja ya Bajeti ya ziada (Supplimentary Budget). Miradi hiyo ni hii ifuatayo:

    i. Mradi wa kilimo cha mpunga cha umwagiliaji maji unaofadhiliwa na Benki ya Exim ya Korea;

    ii. Mradi wa barabara za kuingia mjini unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB);

    iii. Mradi wa Ujenzi wa Bandari mpya ya Mpigaduri chini ya ufadhili wa Benki ya Exim ya China;

    iv. Mradi wa e-government awamu ya pili.

    v. Mradi wa Kuimarisha Elimu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia;

    vi. Mradi wa Huduma za Mijini awamu ya pili chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia; na

    vii. Mradi wa Kuimarisha Nishati na Mafuta na Gesi Asilia unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

49. **Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji wa fedha za Misaada ya Kibajeti (GBS) bado hauna uhakika. Hivyo, kama ilivyokuwa kwa mwaka unaomalizika wa fedha, chanzo hiki kitaendelea kutoingizwa moja kwa moja katika mapendekezo ya mapato na badala yake nacho kuingizwa kwa utaratibu wa 100T.

50. **Mheshimiwa Spika**, Kwa muhtasari, kutokana na maelezo ya hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Serikali inatarajia kukusanya jumla ya TZS 841.5 bilioni zikiwemo TZS 482.4 bilioni zitokanazo na vianzio vya ndani, mikopo ya ndani ni TZS 33.0 bilioni, TZS 324.8 bilioni za kutoka nje, na TZS 1.3 bilioni misamaha ya madeni.

Mwelekeo wa Matumizi

51. **Mheshimiwa Spika**, Kutokana na mwelekeo wa hali ya fedha (fiscal capacity), sera kuu ya matumizi inahitaji kubana zaidi matumizi kulingana na vyanzo vya mapato vilivyopo. Kutokana na mwelekeo huo, mkazo katika matumizi utalenga katika mambo yafuatayo:

    i. Kumaliza/kupunguza madeni hasa ya kiinua mgongo, walimu, wazabuni na Dhamana za Hazina;

    ii. Kuendeleza jitihada za uimarishaji wa huduma za jamii hasa elimu, afya na upatikanaji wa maji safi na salama;

iii. Kutekeleza miradi mikubwa na yenye tija kama vile ukamilishaji wa jengo jipya la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa A.A. Karume na barabara ya Chake – Wete na nyenginezo; na

iv. Utekelezaji wa Mpango wa mageuzi ya Kiuchumi.

52. Mheshimiwa Spika, Serikali pia itaendelea na jitihada zake za kuwaenzi wazee kwa kuendelea kutoa pencheni maalum (universal pension) kwa wazee waliofikia umri wa miaka sabini na zaidi. Napenda kulitangazia Baraza lako Tukufu kuwa **Serikali imeshaanza kuwalipa wazee hao Unguja na Pemba, pencheni ya shilingi 20,000/= kwa kila mwezi kuanzia mwezi Aprili mwaka huu (2016)**. Jitihada hizi ni endelevu katika kutunza hali na kuimarisha maslahi ya wazee wetu.

53. **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na dhamira ya kubana matumizi, Serikali pia imekusudia kutekeleza ahadi yake ya kuimarisha maslahi ya Wafanyakazi wake, hususan wa kipato cha chini, ili waweze kumudu vyema maisha na kuhamasika kufanya kazi kwa bidii zaidi. Bajeti inayopendekezwa inakusudia kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Ali Mohamed Shein ya **kupandisha kima cha chini cha mshahara kutoka TZS 150,000 cha sasa hadi TZS 300,000** katika mwaka wake wa kwanza wa kipindi hiki cha pili cha uongozi wake.

54. **Mheshimiwa Spika**, Naomba nitamke rasmi kuwa marekebisho hayo ya mshahara yatafanyika kuanzia mwezi April 2017. Kama ilivyoahidiwa, nyongeza hii itanufaisha zaidi wafanyakazi wa kada za chini ambao ndio walio wengi. Hatua hii itasaidia pia kuimarisha maslahi ya wafanyakazi hao wakati wanapomaliza utumishi wao kwa kustaafu.

55. **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia imesikia kilio cha wafanyakazi cha kupunguziwa kodi katika kipato cha mshahara na kuwekwa sawa viwango vyake na Tanzania Bara. Hivyo, sambamba na hatua ya kupandisha kima cha chini cha mshahara, kuanzia mwezi huo wa April 2017, **Serikali pia itafanya marekebisho ya Kodi ya Mapato kwa kupunguza kiwango wanachotozwa watu wa kipato cha chini kutoka asilimia 13 ya sasa hadi kufikia asilimia 9.** Lengo la hatua hii ni kuimarisha kipato cha mfanyakazi wa kima cha chini kwa kumbakishia kipato zaidi ili kukidhi mahitaji ya maisha.

56. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inachukua hatua hizi ikielewa mzigo mkubwa inaobeba wa kibajeti. Athari ya hatua hii sio tu kuongeza sana Bajeti ya mishahara na hivyo kupunguza uwezo wake katika matumizi mengineyo na yale ya kazi za maendeleo. Hatua hii itaongeza pia gharama za kiinua mgongo na pencheni kwa Serikali na kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF). Jawabu la athari hizi ni kwa wafanyakazi nao kujituma zaidi na kwa ufanisi ili kuongeza tija,

kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kwa ujumla kukuza kwa haraka zaidi uchumi wetu na hivyo kuongeza wigo wa mapato ya Serikali.

57. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia malengo makuu ya Serikali na mustakabali wa Bajeti, kwa mwaka ujao wa fedha, inatarajiwa kuwa katika kila Shilingi inayotumika, senti 58.7 ziende katika Sekta tano zinazobeba malengo makuu ya Serikali ambazo ni Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji; Elimu na Mafunzo ya Amali; Afya; Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira; na Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kwa ujumla, Sekta hizi tano zinatarajiwa kutumia jumla ya TZS 494.2 bilioni kati ya TZS 841.5 bilioni za matumizi ya Serikali yote.

58. **Mheshimiwa Spika**, Uamuzi huo wa Serikali wa kuelekeza fedha zake nyingi katika sekta hizo una sababu maalum. Kwanza, tunahitaji kuendeleza uwekezaji katika miundombinu yetu ya msingi ili kuwa chachu ya maendeleo yetu ya kiuchumi na kijamii. Asilimia 22.4 ya Bajeti inaelekea katika Sekta hiyo. Pili, huduma za Elimu na Afya nazo pia zina umuhimu wa kipekee katika maendeleo ya wananchi.

59. **Mheshimiwa Spika**, Takwimu zinaonesha ongezeko la wanafunzi katika elimu ya msingi kutoka wanafunzi 233,883 mwaka 2014 hadi 239,274 mwaka 2015. Kwa elimu ya Sekondari, idadi hii nayo imeongezeka kutoka wanafunzi 74,868 hadi 79,608. Kwa upande wa afya, takwimu zinaonesha mafanikio kwa mwaka 2015

kwani idadi ya wagonjwa waliotibiwa katika hospitali za Serikali imepungua kutoka 440,201 mwaka 2014 hadi 438,973 mwaka 2015 wakati idadi ya vifo ikipungua kutoka 1,864 hadi 1,700 katika kipindi hicho. Pamoja na mafanikio haya, bado tuna jukumu la kuendelea kuimarisha huduma za jamii na afya ili kuwaondolea wananchi mzigo wa maradhi.

60. **Mheshimiwa Spika**, Kama nilivyoeleza awali, Serikali inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 482.4 bilioni kutokana na mapato ya ndani katika mwaka wa fedha 2016/17. Kati ya Mapato hayo, jumla ya TZS 32.1 bilioni ni mapato ambayo yameanzishwa kisheria na hivyo hayawezi kuingizwa katika mapato ya jumla ya matumizi. Mapato haya ni pamoja na ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara zetu, Mfuko wa Miundombinu, matumizi ya Bodi ya Mapato (ZRB) na mapato maalum kwa ajili ya utengenezaji wa madawati. Ukiondoa mapato hayo, Serikali inabaki na TZS 450.3 bilioni.

61. **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia inakabiliwa na mtumizi mengine ya kisheria na ya lazima, ambayo kwa mwaka ujao wa fedha yanatarajiwa kufikia TZS 404.4 bilioni yakihusisha mishahara (pamoja na ruzuku) TZS 251.1 bilioni, matumizi ya lazima ya Mfuko Mkuu wa Serikali TZS 59.3 bilioni, matumizi kwa Miradi ya Maendeleo TZS 58.0 bilioni, Elimu (Elimu ya Juu, Baraza la Mitihani na gharama kwa Elimu ya Msingi) TZS 19.5 bilioni, Pencheni kwa

Wazee TZS 6.5 bilioni, Ununuzi wa Dawa TZS 4.5 bilioni pamoja na matumizi mengine ya lazima ya TZS 5.5 bilioni. Kwa ujumla, baada ya matumizi hayo ya kisheria na lazima Serikali itabaki na TZS 49.4 bilioni tu kutokana na mapato yake ya ndani.

62. **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mapato ya Msamaha wa Madeni wa TZS 1.3 bilioni, bado kutakuwa na salio la TZS 46.1 bilioni wakati mahitaji yaliyobakia ya matumizi yanahitaji jumla ya TZS 80.4 bilioni, na hivyo kuacha nakisi ya TZS 33.0 bilioni. Inapendekezwa kukopa kiasi hicho cha fedha kutoka ndani ili kuziba nakisi hiyo.

H. HATUA ZA KUBANA MATUMIZI

Matumizi ya Kawaida

63. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia mwenendo wa mapato na ukuaji wa mahitaji ya matumizi, Serikali inaelewa kuwa haina budi kuimarisha usimamizi wa mapato pamoja na kuimarisha ufanisi katika matumizi. Ni lazima kuhakikisha kuwa fedha zinazotumika zinaleta tija kubwa zaidi. Kwa dhamira hii, ni muhimu kuchukua hatua makhsusi za kukata matumizi yasiyokuwa ya lazima.

64. **Mheshimiwa Spika**, Tayari Serikali imetoa muongozo wa hatua kadhaa zinazolenga kudhibiti zaidi matumizi. Miongoni mwa maeneo ya hatua hizo ni haya yafuatayo:

i. Kusitisha safari zote za nje zisizo na tija;

ii. Kusitisha malipo kwa ajili ya semina, mikutano, warsha na kongamano;

iii. Kusitisha malipo ya posho kwa watumishi wa umma kwa kazi zinazofanywa ndani ya saa za kazi;

iv. Kuzuia matumizi kwa chakula kwa viongozi na watumishi wa umma wakiwa kazini;

v. Kupiga marufuku fedha za Serikali kutumika kulipia watumishi wa umma kupiga kambi katika hoteli kwa ajili ya kufanya "kazi maalum";

vi. Kuelekeza udhibiti katika ununuzi wa vifaa vya kuandikia na mafuta; na

vii. Kuelekeza udhibiti wa matumizi kwa ajili ya sherehe, maadhimisho na machapisho yasiyo ya lazima.

Kutekeleza miradi ya maendeleo yenye tija zaidi

65. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikitekeleza miradi mingi ya maendeleo kwa wakati mmoja na hivyo kutawanya sana rasilimali chache na hivyo kucheleweshа kupatikana tija kubwa. Mapendekezo ya Bajeti ya mwaka 2016/17 yamelenga kuanza kutekeleza agizo la Serikali la kuandaa miradi

michache yenye tija na ambayo ni kipaumbele kwa huduma za jamii na mageuzi ya kiuchumi.

Kudhibiti gharama kutokana na kuanzishwa Taasisi mpya

66. **Mheshimiwa Spika**, Idara nyingi za Serikali zimekuwa zikibadilishwa muundo wake na kuwa Taasisi zenye kujitegemea. Sheria nyingi za Taasisi hizo huhitaji Fungu binafsi (Vote) au zenye kuingiziwa fedha kwa njia ya ruzuku. Aghalabu Taasisi hizo huwa na mifumo mipya ya kiutawala, kufanya ajira mpya na kuendeshwa kwa gharama kubwa zaidi za mishahara kuliko zilizopo katika utumishi wa umma wa kawaida. Serikali itaangalia tena eneo hili na kuzingatia uwezo wa kujitegemea kwa Taasisi hizo au umuhimu mkubwa sana wa Taasisi hizo ambao unafanya majukumu yake yasiweze kutekelezeka kiidara. Vyenginevyo, uanzishwaji wa matumizi ya vifungu vipya utaakhirishwa hadi pale hali ya mapato itakaporuhusu.

Matumizi ya kodi ya miundombinu (infrastructure Tax)

67. **Mheshimiwa Spika**, Wakati wa kuanzisha Mfuko wa Miundombinu, ilikubalika kuwa asilimia 75 ya Kodi ya Miundombinu iliyoanzishwa mwaka jana itumike kwa madhumuni ya miundombinu na asilimia 25 iliyobakia itumike kwa mifuko mingine kadhaa iliyotajwa katika Sheria mbalimbali. Kutokana na

mahitaji makubwa ya miundombinu na dhamira ya Serikali ya kuleta maendeleo ya haraka, inapendekezwa kwamba kodi yote ya miundombinu itumike katika shughuli za uimarishaji wa miundombinu pekee. Matumizi ya mifuko mingine yaendelee kuwa sehemu ya matumizi mengineyo ya Wizara husika na Mfuko Mkuu wa Hazina kwa wakati wa dharura.

68. **Mheshimiwa Spika**, Sambamba na pendekezo hilo, inapendekezwa zaidi kuwa kwa mwaka ujao wa fedha, jumla ya TZS 26.6 bilioni kutoka Mfuko wa Miundombinu zitumike kugharamia miradi ya miundombinu ifuatayo:

i. Uwekaji wa Kamera za Vifaa vya Ulinzi - TZS 18 bilioni;

ii. Ujenzi wa barabara za Pemba (Chake - Wete na Ole - Kengeja) – TZS 1.7 bilioni;

iii. Usambazaji wa Umeme vijijini (kisiwa cha Fundo) – TZS 2.0 bilioni;

iv. Uimarishaji wa Elimu ya msingi, elimu Mbadala na Amali – TZS 1.6 bilioni;

v. Mradi cha mpunga cha Umwagiliaji – TZS 400 milioni;

vi. Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Ufugaji – TZS 140 milioni;

vii. Mradi wa Kuimarisha ufugaji wa Mazao ya Baharini – TZS 100 milioni;

viii. Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango ya Zanzibar – TZS 1.0 bilioni;

ix. Mradi wa "Business Incubator" – TZS 400 milioni;

x. Mradi wa Kuimarisha Huduma za Uzamiaji na Uokozi (hyperbaric chamber) – TZS 400 milioni; na

xi. Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali – TZS 500 milioni.

I. HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO

69. **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuzipongeza na kuzishukuru Taasisi za ukusanyaji wa mapato, TRA, ZRB na Wizara mbalimbali, Serikali inaamini kuwa bado kuna fursa ya kukusanya mapato zaidi kutokana na vyanzo vya ndani kuliko kiasi kinachokusanywa sasa. Kwa sababu hii, kwa mwaka ujao wa fedha (2016/17) haipendekezwi kupandisha kodi yoyote katika vianzio vyake vya mapato ya ndani, zaidi ya kurekebisha viwango vya ada mbalimbali vilivyopitwa na wakati. Badala yake, inashauriwa kuendelea na hatua makhsusi za kupanua wigo wa kodi, kuimarisha ufanisi katika ukusanyaji, na kuongeza uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato.

70. **Mheshimiwa Spika**, Mkazo huu unaendana na dhamira ya Serikali ya kuwa na Bajeti yenye kujitegemea kwa kupunguza utegemezi wa misaada ya ruzuku kutoka nje kama nilivyoeleza awali. Hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa ni pamoja na hizi zifuatazo:

Uanzishaji na usimamizi wa maeneo maalum ya kikodi (Block Management System):

71. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato (TRA) na Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) zinafanya kazi kwa pamoja ili kuigawa Zanzibar katika maeneo maalum ya kikodi. Lengo la hatua hii ni:

    i. Kuweza kuwabaini walipa kodi wote wa kila eneo na kuwasajili katika mtandao wa kodi;

    ii. Kubaini fursa zote zilizopo kwa kodi mbalimbali katika kila eneo;

    iii. Kuwezesha mapato yote ya Serikali kutambuliwa na kukusanywa kwa urahisi zaidi; na

    iv. Kuongeza ufanisi wa ukusanyaji kwa kuhakikisha kuwa Taasisi hizi mbili zinawasajili walipakodi walewale na hivyo kuwezesha kodi zote kukusanywa.

72. **Mheshimiwa Spika**, Utaratibu huu unakusudiwa kuongeza ufanisi na uwajibikaji kwa kuimarisha usajili

wa wafanyabiashara wote kupitia Mrajis wa Biashara, matumizi ya TEHAMA, na wafanyakazi wa TRA na ZRB kugaiwa maeneo makhsusi (blocks) ya kusimamia.

Kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya kodi ya ardhi na majengo (Property Tax):

73. **Mheshimiwa Spika**, Kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Wathamini wa Majengo, ukusanyaji wa Kodi hii unakusudia kuanza rasmi mwaka 2016/17 mara tu utekelezaji wa Sheria hiyo utakapoanza. Kwa kuanzia, kodi hiyo itakusanywa katika majengo yanayotumika kwa biashara.

Kuyafanyia kazi mapendekezo ya kuongeza mapato yaliyoibuliwa katika maabara ya mapato:

74. **Mheshimiwa Spika**, Utakumbuka kuwa katika Mpango wa "Matokeo kwa Ustawi – R4P", moja ya eneo lililowekewa mikakati ni la utafutaji wa mapato ya ndani. Mikakati hiyo itaendelea kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha.

Kuongeza udhibiti wa misamaha ya Kodi:

75. **Mheshimiwa Spika**, Misamaha ya kodi isiyo na tija inaathiri uwezo wa Serikali kutoa huduma bora zaidi kutokana na kupunguza uwezo wake kifedha wakati ikinufaisha watu wachache. Serikali itaendelea kudhibiti utoaji wa misamaha ya kodi pamoja na kuzuia matumizi mabaya kwa ile misamaha inayotolewa.

Kupambana na magendo ya mafuta:

76. **Mheshimiwa Spika**, uingizaji wa aina mbalimbali za mafuta ya petroli ni eneo muhimu la mapato ya Serikali. Kuendelea kwa magendo ya mafuta hayo kunaendelea kuathiri mapato ya Serikali. Hatua zaidi za udhibiti wa magendo hayo zitaendelezwa ikiwemo kudhibiti mauzo ya mafuta nchini, katika vituo rasmi na visivyo rasmi.

Hatua za Kiutawala

77. **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa hatua za kiutawala, maeneo yatakayosimamiwa kwa karibu ni pamoja na haya yafuatayo;-

Ada ya Ukaguzi wa Bidhaa katika kituo (Destination Inspection Fee) na Uthibitishaji wa Bidhaa (Customs Declaration-TANSAD)

78. **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Forodha nchini imekuwa ikitoza ada ya ukaguzi wa bidhaa katika kituo (Destination Inspection Fee) kwa asilimia 0.6 ya thamani ya bidhaa iliyoingizwa na Ada ya Uthibitishaji wa Bidhaa (Customs Declaration-TANSAD) ambayo ni 10 USD kwa kila kadhia ya Forodha. Mapato kutokana na ada hizi hubakishwa Idara ya Forodha kwa dhamira ya kuijengea uwezo na kuleta mageuzi.

79. **Mheshimiwa Spika**, Ada hizi hazitozwi hapa Zanzibar na kuifanya Idara hiyo kuendelea kusubiri mgao wa Fedha kutoka makao makuu. Inapendekezwa kutoza ada hizo hapa Zanzibar kuanzia tarehe 1 Julai 2016 na kuziweka katika mfuko maalum (Basket Fund). Mapato kutoka mfuko huo yatumike katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani nchini kote, ikiwemo uimarishaji wa Idara ya Forodha (mordernization), Idara ya Mapato ya Ndani ya TRA na utekelezaji wa Mpango Mkuu wa ZRB. Hatua hii inatarajiwa kuingiza jumla ya TZS 6.68 bilioni.

Vibali vya Kodi kwa Wazabuni (Income Tax Clearance Certificate)

80. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuwa ni mnunuzi mkubwa wa bidhaa na huduma, kupitia

zabuni mbalimbali. Kwa bahati mbaya, katika ununuzi huu, baadhi ya Wazabuni wanaofanya biashara na Serikali hawalipi kodi ipasavyo. Muongozo maalum utatolewa kwa kila Wizara, Idara inayojitegemea na Taasisi zote za Serikali zisitowe zabuni kwa wazabuni wasiokuwa na uthibitisho wa kulipa kodi (Tax Clearance Certificates) kutoka ZRB na TRA.

Usajili wa Jina la Biashara (Business Registration Name)

81. **Mheshimiwa Spika**, Kutokana na kufanana kwa majina ya wafanyabiashara wadogo wadogo kunakopelekea ugumu wa kutambulika katika Taasisi za kodi (TRA & ZRB), wafanyabiashara wote nchini watatakiwa kusajili jina la biashara kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya Serikali. Hatua hii itakwenda sambamba na uimarishaji wa usimamizi wa kimaeneo (Block Managamenet System) ulioelezwa hapo kabla.

Usimamizi wa mapato kutokana na Ardhi:

82. **Mheshimiwa Spika**, Bado kuna fursa kubwa ya kuongeza mapato kutokana na matumizi ya ardhi. Kumeanza pia kujitokeza miradi mikubwa ya uwekezaji katika ujenzi wa nyumba kwa ajili ya kukodisha na kuuza (real estate). Kwa ujumla, matumizi ya ardhi yanajitokeza kuwa chanzo muhimu

sana cha uchumi. Wizara ya Fedha na Mipango inaendelea na matayarisho maalum kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira yanayokusudia kuhakikisha kuwa uchumi huu unaotumia moja kwa moja ardhi unachangia ipasavyo katika mapato ya Serikali.

Uhaulishaji magari kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara

83. **Mheshimiwa Spika**, Kumekuwa na biashara kubwa ya uingizaji wa gari nchini na baadae kuhaulishwa kwenda Tanzania Bara. Kwa sasa pande mbili hizi za Jamhuri ya Muungano zinatumia mifumo tofauti ya uthamini wa kodi za magari unaopelekea gari hizo kutozwa tofauti kubwa ya ushuru na kodi pale zinapohaulishwa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Kuanzia Julai 2016, Mamlaka ya Mapato Tanzania-Zanzibar itakadiria na kukusanya tofauti yote ya kodi kabla ya gari kuhaulishwa kwenda Tanzania Bara.

Usajili wa Vyombo vya Moto

84. **Mheshimiwa Spika**, Suala la usajili la vyombo vya moto sio la Muungano. Kila upande wa Jamhuri una utaratibu wake wa kisheria wa kusajili vyombo hivyo. Kwa sababu hii, ukiacha vyombo vya Serikali, vyombo vilivyosajiliwa Zanzibar haviruhusiwi

kutembea Tanzania Bara kwa namba za Zanzibar. Ili kuleta usawa katika utekelezaji wa Sheria na usajili, kuanzia tarehe 01 Julai 2016, vyombo vya moto vyenye usajili wa Tanzania Bara vitapaswa kusajiliwa upya Zanzibar kama vyombo vyengine vyote vinavyotoka nje ya nchi.

SURA YA BAJETI

85. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na maelezo ya hapo juu, Sura ya Bajeti ya mwaka 2016/17 inahusisha mapato ya jumla ya TZS 841.5 bilioni, ikiwemo Mapato ya Ndani ya TZS 482.4 bilioni, Mapato kutoka nje ya TZS 324.8 bilioni, fedha kutokana na Misamaha ya Madeni ni TZS 1.3 bilioni na Mikopo ya ndani ya TZS 33.0 bilioni. Kwa upande wa matumizi, kiasi hicho cha TZS 841.5 bilioni kinatarajiwa kugawanywa kwa TZS 445.6 bilioni kuelekezwa katika matumizi ya kazi za kawaida na TZS 395.9 bilioni kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

86. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia kuwa kati ya fedha zote za TZS 841.5 bilioni, Ruzuku kutoka nje inatarajiwa kufikia TZS 93.3 bilioni tu, hali hii inamaanisha kuendelea kupungua kwa utegemezi wa ruzuku kutoka nje hadi kufikia asilimia 11.1 ya Bajeti ya Serikali, ikimaanisha kupungua zaidi kutoka asilimia 12.2 ya mwaka 2015/16. Hali hii inaashiria kuwa tupo katika njia sahihi ya kupunguza utegemezi kwa utekelezaji wa Bajeti yetu.

MFUMO WA BAJETI 2016/17				
Maelezo	**Makisio 2015/16**	**Matarajio Hadi June 2016**	**Makisio 2016/17**	**Ongezeko/ Punguzo la (%)**
MAPATO				
A Mapato ya ndani	429.5	391.5	461.4	*7.4*
B 4.5% Msaada wa kibajeti (GBS)	100T	7.7	100T	-
C Kodi ya Mapato kwa W/Kazi wa SMT	21.0	21.0	21.0	*0.0*
C Dhamana za Hazina na Hati Fungani	30.0	10.0	33.0	*10.0*
F Msamaha wa Madeni (MDRI)	1.3	0.0	1.3	*0.0*
G Mikopo na Ruzuku	347.1	84.3	324.8	*-6.4*
H Mfuko wa Wafadhili (BF)	1.5	1.5	0.0	-
Jumla ya Mapato	**830.4**	**516.0**	**841.5**	***1.3***
MATUMIZI				
Matumizi ya Kawaida	**431.4**	**399.1**	**445.6**	***11.7***
i) Mishahara (Wizara)	205.8	196.0	223.7	*8.7*
ii) Mishahara (Ruzuku)	28.6	30.0	27.4	*-4.2*
iii) Matumizi Mengineyo (Wizara)	84.3	65.6	80.6	*-4.4*
iv) Matumizi Mengineyo (Ruzuku)	28.5	23.3	31.6	*10.9*
v) Mfuko mkuu wa Serikali (CFS)	84.2	84.2	82.3	*-2.2*
Matumizi ya Maendeleo	**399.1**	**116.9**	**395.9**	***-0.8***
i) Mchango wa Serikali	51.9	32.6	71.1	*37.0*
ii) Ruzuku	98.3	44.0	93.3	*-5.1*
ii) Mikopo	248.9	40.3	231.5	*-7.0*
Jumla ya matumizi	**830.4**	**516.0**	**841.5**	***1.3***

***Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango*

J. SHUKRANI

87. **Mheshimiwa Spika**, Matayarisho haya ya Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali yameshirikisha Taasisi na watu mbalimbali. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wote ambao kwa namna moja au nyengine wameshiriki katika kufanikisha mapendekezo haya. Naomba niwashukuru sana

Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza lako hili tukufu kwa kuyapitia mapendekezo haya kwa kina na hatimae kutoa muongozo wa Kamati na kuridhia yawasilishwe katika Baraza hili.

88. **Mheshimiwa Spika**, Namshukuru pia Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu wote kwa kuyapitia mapendekezo ya awali kabla ya kuwasilishwa Baraza la Mapinduzi na kufanya marekebisho kwa mujibu wa maelekezo ya Baraza la Mapinduzi yaliyowezesha Mapendekezo haya kuwasilishwa leo hii hapa Barazani.

89. **Mheshimiwa Spika**, Shukrani za pekee ni kwa watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiwemo wa Tume ya Mipango kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kipindi kifupi. Niruhusu, kwa niaba yao, niwashukuru sana Bwana Khamis Mussa Omar, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Bwana Juma Hassan Reli, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Bwana Ali Khamis Juma, Naibu Katibu Mkuu – Fedha na Mipango, Bwana Mwita Mgeni Mwita Kamishna wa Bajeti, Makamishna, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi kubwa iliyofanikisha mapendekezo haya kusomwa leo hapa.

90. **Mheshimiwa Spika**, Kwa nafasi hii pia nampongeza Bi Mwanahija Almasi Ali kwa kuteuliwa na

Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kushika wadhifa wa Mhasibu Mkuu wa Serikali. Namshukuru sana mtangulizi wake Bwana Omar Hassan Omar na kumtakia utendaji bora katika nafasi yake mpya.

91. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kufanya kazi kwa karibu na nchi rafiki na Mashirika ya kimataifa. Naomba kushukuru sana mashirikiano na msaada wa nchi za Canada, China, Cuba, Denmark, Falme za Kiarabu, Finland, India, Ireland, Japani, Korea ya Kusini, Kuwait, Marekani, Misri, Norway, Oman, Saudi Arabia, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uturuki.

92. **Mheshimiwa Spika**, Naomba nitambue na kushukuru misaada ya mashirika yafuatayo ambayo nayo tumeendelea kufanya nayo kazi kwa karibu: ACBF, ACCRA, AfDB, AGRA, BADEA, CARE INTERNATIONAL, CDC, CHAI, CIDA, DANIDA, DFID, EGH, EU, EXIM Bank ya China, EXIM Bank ya Korea, FAO, FHI, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, IAEA, ICAP, IDB, IFAD, ILO, IMF, IPEC, JICA, JSDF, KOICA, MCC, NORAD, OFID, ORIO-Netherlands, PRAP, SAUDI FUND, Save the Children, SIDA, UN AIDS, UN, UNDP, UNESCO, UNFPA, UN-HABITAT, UNICEF, UNIDO, USAID, WB, WHO na WSPA .

K. HITIMISHO:

93. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo ya hapo juu, naomba sasa Baraza lako tukufu liidhinishe mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 yenye mapato ya jumla ya TZS 841.5 bilioni zikiwemo TZS 482.4 bilioni za mapato ya ndani, TZS 324.8 bilioni kutokana na Ruzuku na Mikopo kutoka nje, TZS 1.3 bilioni kutokana na misahama ya madeni (MDRI) na TZS 33.0 bilioni za mikopo ya ndani. Aidha, tunaomba Baraza liidhinishe matumizi ya 841.5 bilioni ikiwa ni TZS 445.6 bilioni kwa matumizi ya kawaida na TZS 395.9 bilioni kwa kugharamia Mpango wa Maendeleo.

94. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Dkt. Khalid S. Mohamed,
Waziri wa Fedha na Mipango,
Zanzibar.

18 Mei, 2016.